Kiambatisho Na. 1

**UTARATIBU UTAKAOFUATWA NA MKUSANYAJI MAZAO (MFANYABIASHARA) AMBAYE ATARUHUSIWA KUPELEKA MAZAO GHALA KUU KAMA MWEKA MALI KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA NA MINADA YA KIDIJITALI KWA MWAKA 2026.**

**Angalizo;**

1. Utaratibu huu utatumika katika mikoa ya Dodoma, Manyara, Simiyu, Shinyanga, Arusha na Mwanza.
2. Mkusanyaji mazao/mkulima mkubwa hataruhusiwa kuwa Mwendesha Ghala.
3. Mkusanyaji mazao atakayesajiliwa kupitia Mwongozo huu, atahesabika kuwa ameridhia kuwa atahitajika kusaini hati ya ridhio la bei ndani ya saa moja toka kumalizaka kwa mnada. Iwapo hatasaini hati hiyo, mzigo utahesabika kuwa umeuzwa.
4. Mkusanyaji mazao (Mfanyabiashara) atafutiwa usajili na Mamlaka ya udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko iwapo atashindwa kufuata taratibu zilizowekwa katika Mwongozo wa biashara Toleo 5-2026 wa mazao ya choroko, dengu, mbaazi, soya, njugumawe, kunde, ufuta na karanga pamoja na utaratibu huu na hivyo hataruhusiwa kufanya biashara yoyote ya nafaka na mazao mchanganyiko.

## TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA

**Ghala Kuu:**

Maana yake ni ghala liliiosajiliwa na Bodi ya usimamizi wa Ghala kwa mujibu wa Sheria Sura namba 339 (RE 2016)lililokidhi sifa na vigezo kwa ajili ya kukusanya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi, Njugumawe, Kunde, Dengu na Karanga za wakulima/waweka mali yatakayouzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

**Mwendesha ghala/Mtunza Ghala:**

Kampuni iliyosajiliwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kujishughulisha na biashara ya kuendesha ghala kwa lengo la kupokea na

Kuhifadhi mazao jamii ya mikunde na mazao jamii ya mafuta kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura ya 339(RE 2016)

**Mkusanyaji Mazao:**

Maana yake ni mfanyabiashara mwenye jukumu la kununua mazao kutoka kwa mkulima katika maeneo ambayo yamethibitika kutokuwa na ushirika imara wenye uwezo wa kuhudumia wakulima. Mkusanyaji mazao atasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura 249 iliyofanyiwa Urekebu mwaka 2023.

**Mnunuzi**

Maana yake ni wakala, muuzaji, kampuni au mnunuzi aliyesajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) kwa lengo la kununua na kuuza nafaka au mazao mengine mchanganyiko kutoka kwa mzalishaji kwenye maeneo ambayo yamethibitika kutokuwa na ushirika imara kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura 249 iliyofanyiwa urekebu mwaka 2023.

**Timu ya usimamizi**

Kikosi kazi jumuishi cha ukaguzi kitakachoundwa na COPRA kwa mujibu wa Kanuni za Udhibiti Ubora wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko za mwaka 2026 kifungu cha 14 (d) chini ya Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura 249 (RE 2023).

**Msafirishaji wa bidhaa/mazao**

Ni wakala au kampuni iliyosajiliwa inayohusika na usafirishaji wa mazao kutoka au kwenda kwenye ghala lililosajiliwa, kwa kutumia stakabadhi za ghala kama nyaraka halali ya uthibitisho wa umiliki na idhini.

**VIGEZO VYA KUMSAJILI MKUSANYAJI MAZAO (MFANYABIASHARA)**

i. Katika kuhakikisha mfumo wa Stakabadhi za Ghala unatekelezwa kwa ufanisi na kwa kufuata utaratibu kulingana na mwongozo wa mwaka 2026, Mamlaka ya udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko itamtambua mkusanyaji mazao, vituo vya kukusanyia mazao na kuwapatia usajili kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura 249 katika Kifungu cha 14(1).
ii. Ili kusajiliwa mkusanyaji mazao atatakiwa awe na uwezo wa kukusanya mazao kuanzia tani 30.
iii. Ili kusajiliwa Mkusanyaji mazao atatakiwa kuwasilisha;
    a. Barua ya utambulisho kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ikiwa imepitishwa na Chama cha Wafanyabiashara katika Wilaya husika.
    b. Nakala ya Cheti cha usajili wa Kampuni (iwapo anamiliki kampuni) au

nakala ya kitambulisho cha NIDA,

c. Leseni ya biashara ya Halmashauri atakapofanya biashara,

d. Nakala ya Namba ya Mlipa kodi (TIN),

e. Kuwasilisha eneo la kununulia mazao (Halmashauri za wilaya, kijiji na mahali husika) na ghala lenye usajili atakapouzia mazao yake,

f. Taarifa za benki kwa ajili ya kupokea malipo na bank statement kuthibitisha uwezo wake, na

g. Uthibitisho wa uwezo wa kufanya biashara ya kukusanya mazao kutoka kwa wakulima.

iv. Mkusanyaji mazao atajisajili kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha https://portal.copra.go.tz/portal/

v. Mkusanyaji mazao atakuwa mweka mali kwenye ghala maalum liliothibitishwa na mamlaka inayosimamia maghala kama ilivyo kwa wakulima waliokusanya kupitia vyama vya ushirika. Aidha, mkusanyaji mazao hataruhusiwa kufanya jukumu la ukaguzi na uendeshaji wa ghala. Endapo itabanika kuwa mkusanyaji mazao amejihusisha na ukaguzi na uendeshaji wa ghala hatua stahiki zitachuliwa ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili;

vi. Ghala zitakazotumika katika utekelezaji wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa mfumo wa ukusanyaji mazao zitapaswa kusajiliwa na WRRB na COPRA kwa kuzingatia sheria na kanuni za mamlaka husika.

vii. Kila mkusanyaji mazao atapaswa kuwa na vituo vya kukusanyia mazao visivyozidi nane (08) vinavyotambulika ndani ya Halmashauri husika.

viii. Pia, Sheria ya Stakabadhi za Ghala kifungu 33(1)(g) inaainisha aina za umiliki wa Mazao yanayo hifadhiwa ghalani kuwa unaweza ukahusisha Kikundi "Common Owned"' au Mtu mmoja "Solely" au wa Pamoja wenye uwiano sawa wa umiliki "Joint Ownership".

## 1.1 Utaratibu wa ukusanyaji, uhifadhi na uuzaji

i. Mkusanyaji mazao atatakiwa kuwa na vituo vya kukusanyia/ kununulia mazao katika Halmashauri husika vilivyotambuliwa na COPRA.

ii. Mkusanyaji mazao (Mfanyabiashara) atatakiwa kununua mazao kutoka kwa mkulima **kwa bei isiyopungua asilimia 85 ya bei ya mnada uliofanyika ndani ya masaa 24 kabla au mnada mwingine wa mwisho wa zao hilo uliofanyika kabla ya manunuzi**. Iwapo Mkusanyaji mazao atanunua mazao chini ya bei anzia atafutiwa usajili wake na hivyo hataruhusiwa kufanya biashara ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko.

**Angalizo1:** bei za minada zitakuwa inatangazwa kila baada ya minada na TMX pamoja na COPRA.

**Angalizo2**: Halmashauri za Wilaya zitatangaza bei inayopatikana katika minada kila

mara kupitia mbao za matangazo katika ofisi ya kata/kijiji/mtaa na maeneo mengine yanayoweza kufikiwa na wakulima.

iii. Mkusanyaji mazao (Mfanyabiashara) atatakiwa kuonesha cheti chenye namba ya usajili kilichotolewa na COPRA kwa mkulima anayeuza mazao.

iv. Kwa ajili ya utambuzi, mkulima anayeuza mazao yake kwa mkusanyaji mazao atatakiwa kunakili namba ya usajili ya mnunuzi iliyoko kwenye cheti kilichotolewa na COPRA pamoja na taarifa za ununuzi na kuwa tayari kuziwasilisha pale zinapohitajika na Mamlaka (COPRA).

v. Mkusanyaji mazao (Mfanyabiashara) atatakiwa kuweka kumbukumbu ya mkulima aliyemuuzia mazao ikiwa na taarifa ya jina la mkulima, kiasi alichomuuzia, tarehe na bei aliyonunulia na kuiwasilisha ghala kuu pamoja na mazao. Pia, nakala yenye rejea ya taarifa ya mzigo na siku ya kupelekwa ghalani itawasilishwa kwa Mamlaka (COPRA) kupitia COPRAMIS;

vi. Mkusanyaji mazao atatakiwa kuhakikisha mazao aliyonunua yako katika hali ya usafi na ubora na yamefungwa katika vifungashio maalumu na vyenye ubora kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa biashara Toleo 5 - 2026 kabla ya kusafirisha kwenda kwenye ghala kuu;

vii. Mkusanyaji mazao mara atakapofikisha mazao yake katika ghala kuu atatakiwa kufuata taratibu zilizowekwa kwenye Mwongozo wa biashara Toleo 5 - 2026 wa mazao ya choroko, dengu, mbaazi, soya, njugumawe, karanga, kunde na ufuta na miongozo mingine ya biashara ya mazao;

viii. Mauzo ya mazao yote yatakayokusanywa na kuhifadhiwa ghalani yatauzwa kwa utaratibu ulioainishwa katika Mwongozo wa biashara Toleo 5-2026 wa mazao ya choroko, dengu, mbaazi, karanga, soya, njugumawe, kunde na ufuta na miongozo mingine ya biashara ya mazao;

ix. Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) litatoa hati ya madai ya malipo kwenda kwa mnunuzi mara baada ya mnada na malipo yote yatafanyika katika akaunti ya malipo "Settlement Account". TMX itahamisha malipo yote Kwenda akaunti za mkusanyaji mazao pamoja na Taasisi na wote waliopo katika mjengeko wa Tozo.

x. Mkusanyaji mazao (Mfanyabiashara) atakuwa na jukumu la kukusanya mazao kutoka kwa wakulima na kupeleka katika ghala lililopewa leseni na hataruhusiwa

kuendesha ghala;

xi. Mwendesha ghala atakuwa na jukumu la kuendesha ghala kwa mujibu wa taratibu zilizoanishwa katika Mwongozo wa Biashara Toleo 5 - 2026;

xii. Wakaguzi wa ghala watakuwa na jukumu la kukagua mazao yaliyohifadhiwa ghalani na kutoa taarifa kwa Mamlaka zinazohusika. Aidha, mdau yeyote kwenye utekelezaji wa mfumo ambaye atashindwa kufuata utaratibu na mwongozo wa biashara atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

xiii. TMX kwa kushirikiana na COPRA itamshirikisha mkusanyaji mazao kumshauri kuhusu bei ya kuanzia “Reserve Price” katika mnada husika kulingana na mwenendo wa soko wa zao husika;

xiv. Mkusanyaji mazao (Mfanyabiashara)/ Mkulima mkubwa atatakiwa kujaza fomu yakuridhia au kutoridhia bei ndani ya saa moja baada ya mnada kufanyika;

xv. Muda ulioainishwa wakuridhia/kutoridhia bei ukipita bila kuwasilisha fomu, bei zilizopatikana zitahesabika kuwa zimekubaliwa na wauzaji na hivyo mazao hayo yatahesabika kuwa yameuzwa;

xvi. Mkusanyaji mazao hataruhusiwa kuzuia mzigo kuchukuliwa na mnunuzi endapo taratibu zote za ununuzi zitakuwa zimefuatwa kulingana na Mwongozo wa Biashara toleo la 5- 2026.

### 1.2 Timu ya Usimamizi

**i.** Kwa mujibu wa Kanuni za Udhibiti Ubora wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko za mwaka 2026 kifungu cha 14 (d) katika mfumo wa wakusanyaji mazao kutakuwa na Kikosi kazi cha ukaguzi kitakachokuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kufanya ufuatiliaji wa mazao yanapokua ghalani ikiwemo uhakiki wa mara kwa mara wa kiasi na ubora wa mazao hayo.
b) Kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa wakusanyaji mazao, wanunuzi na wadau wengine katika utekelezaji wa mwongozo huu. Endapo Timu itagundua changamoto kwenye upande wa waendesha ghala, taarifa itapelekwa kwa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi ghalani kwa hatua stahiki.
c) Kufanya uhakiki wa taarifa za usajili na taarifa za waweka mali (aggregators) katika maghala yanayotumika kuhifadhi mazao.
d) Kufanya ufuatiliaji wa bei anazopata mkulima katika maeneo husika na kulinganisha na bei za mnada
e) Kuhakikisha taratibu za kiuendeshaji katika mwongozo huu zinafuatwa

kiukamilifu.

ii. Timu ya usimamizi itakuwa na wajumbe Sita kama ifuatavyo:

a) Mkuu wa Kanda wa COPRA – Mwenyekiti
b) Mwakilishi kutoka COPRA HQ - Katibu
c) Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya - Mjumbe
d) Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji – Mjumbe
e) Mwakilishi kutoka TMX – Mjumbe
f) Mwakilishi kutoka WRRB - Mjumbe
g) Mwakilishi kutoka Chama cha wafanyabiashara – Mjumbe

iii. Kikosi kazi hiki kitawajibika kwa kutoa taarifa ya utendaji ya kila wiki kwa Mkurugenzi Mkuu wa COPRA.
iv. Kikosi kazi cha ukaguzi kitakuwa kinatekeleza shughuli zake kupitia fedha ya kikosi kazi cha ukaguzi inayokusanywa kupitia mjengeko wa tozo na kuhifadhiwa na COPRA.
v. Kila Taasisi yenye mwakilishi katika kikosi kazi itateua mjumbe wa kudumu katika kikosi na kisha katibu kuitisha kikao cha kwanza ambapo mpango kazi na bajeti zitaandaliwa na kuwasilishwa COPRA kwa ajili ya utekelezaji.
vi. Kikosi kitatakiwa kuhakiki taarifa zote za mauzo hasa yaliyopo katika hati ya mauzo siku moja kabla ya mauzo kufanyika.
vii. Timu hii ni tofauti na kamati ya Wilaya ya usimamizi wa mfumo wa stakabadhi za ghala na kitakoma baada ya msimu kukamilika.

### 1.3 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)

Kwa muktadha wa Mwongozo huu, WRRB itaendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na sheria yake namba 10 ya mwaka 2005 na sura namba 339 iliyofanyiwa urekebu mwaka 2016 pamoja na kanuni zake itatimiza majukumu yake kama yalivyoanishwa katika Mwongozo wa Biashara ya mazao toleo la 5 – 2026. Pamoja na majukumu yake ya Msingi, Bodi itaweka usimamizi wa ziada kwenye maghala kusimamia utekelezaji wa mfumo wa ukusanyaji mazao kupitia wafanyabiashara (aggregator model) kama ifuatavyo;

i. Kuweka msimamizi wa kudumu katika kila ghala la minada kufanya ukaguzi wa ubora na kiasi kwa kila mzigo uliopokelewa na mwendesha ghala. Ukaguzi huu utakuwa unafanywa na afisa wa ubora waliosajiliwa na WRRB Pamoja na afisa wengine kutoka maeneo tofauti kadri itakavyoona inafaa katika ghala muda wote wa upokeaji na upakiaji wa mazao.
ii. Kukagua taarifa za waweka mali wote waliowasilisha mizigo ghalani na kuhakikisha wana usajili halali kama ilivyoainishwa kwenye taarifa za COPRA.
iii. Kupiga picha na video za mzigo ambazo zitapelekwa TMX kuonyesha hali ya

ubora lwa mzigo ili kuchochea upatikanaji wa bei nzuri kwenye minada.

iv. Kumsimamia mwendesha ghala na kuhakikisha anatimiza wajibu wake kwa mujibu wa Mwongozo huu na ule Mwongozo wa Biashara ya Mazao toleo la 5 – 2026.

v. Kuhakiki kila mara mwendesha ghala haweki mzigo katika ghala unaomilikiwa na yeye mwenyewe au kampuni yeyote anayohusiana nayo.

vi. Ili kutekeleza shughuli hizi, WRRB itatumia fedha ya usimamizi wa mfumo wa stakabadhi za ghala zitakazokusanywa kupitia mjengeko wa tozo. Fedha hii itakuwa inahifadhiwa na WRRB.

## 1.4 Mjengeko wa Tozo

**Jedwali Na.1.**Mjengeko wa Tozo kwa mazao ya Ufuta, Dengu, Mbaazi, Soya, karanga na Choroko.

| Na. | Aina ya tozo | Mlipaji wa tozo kwa kila kilo | |
|---|---|---|---|
| | | Mkulima | Mnunuzi |
| 1. | Mtunza Ghala | 00 | 32.5 |
| 2. | Usimamizi wa mfumo wa stakabadhi za ghala | 00 | 6 |
| 3. | Timu ya Usimamizi | 00 | 0.75 |
| 4. | Dhamana ya Utunzaji mazao Ghalani | 00 | 4 |
| 5. | Usafirishaji | 00 | 50 |
| 6. | Usimamizi wa mauzo | 00 | 10 |
| 7. | Usimamizi Mkoa | 00 | 02 |
| 8. | Usimamizi Wilaya | 00 | 02 |
| 9. | Vifungashio | 00 | 20 |
| 10. | Maendeleo ya zao | 00 | 30 |
| 11. | Ushuru wa Halmashauri | 00 | 3% |
| **Jumla ya tozo** | | | **157.25 + 3%** |

**Angalizo;**

Mjengeko wa Tozo baada ya msimu kufungwa utakuwa kama ilivyo katika mwongozo wa biashara **Toleo 5 – 2026 Jedwali Na. 4 & 5**

**Utaratibu huu umetolewa na;**

| | | |
|---|---|---|
| ………………… | ……………………… | ……………………… |
| Irene M.Mlola | Godfrey Malekano | Asangye N. Bangu |
| **MKURUGENZI MKUU MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO** | **AFISA MTENDAJI MKUU SOKO LA BIDHAA TANZANIA** | **MKURUGENZI MTENDAJI BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA** |

**Tarehe ya kutolewa kwa Kiambatisho hiki**……1st June 2026……